

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. ZELOTE  
STEPHEN ZELOTE ALIYOITOA WAKATI WA KUFUNGA MAFUNZO  
YA USALAMA BARABARANI KWA WAENDESHA PIKIPIKI WA  
WILAYA YA SUMBAWANGA YALIYOENDESHWA NA APEC KWA  
KUSHIRIKIANA NA JESHI LA POLISI TAREHE 04 MEI, 2016.**

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,  
Mkurugenzi Mtendaji wa APEC,  
Kamanda wa Polisi Mkoa,  
Viongozi wa Madhehebu ya Dini,  
Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda Wilaya ya Sumbawanga,  
Ndugu Washiriki wa Mafunzo,  
Waandishi wa Habari,  
Wageni waalikwa  
**Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana kwa ajili ya shughuli ya ufungaji mafunzo kwa waendesha Bodadada wa Mjini Sumbawanga siku hii ya leo.

**Ndugu Mwenyekiti wa Bodaboda,**

Kipekee nichukue fursa hii kuwapongezeni waendesha Bodaboda kwa muitikio mzuri kwa ajili ya kushiriki mafunzo haya. Kama inavyofahamika

elimu haina mwisho mmejitendea haki kwa kushiriki na kuweza kupata mafunzo haya.

Aidha, napenda kutoa pongezi za dhati na kuwashukuru viongozi wa APEC na watoa mada kwa kuwezesha mafunzo haya kufanyika ndani ya Mkoa wetu, mafunzo haya yana faida kwetu kwa kuwa yatapunguza changamoto za barabarani katika Mkoa wetu.

### **Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana,**

Nashukuru kwa taarifa na Risala nzuri ambayo imejikita katika kuelezea changamoto zilizopo ambazo kwa namna moja au nyingine zinaikabili Sekta hii ya usafirishaji hususan vijana wetu waendesha bodaboda.

- Suluhu kubwa ya kukabiliana na changamoto ni kufuata sheria
- Kujichukulia sheria mkononi kutaongeza uwingi wa changamoto au matatizo katika sekta hii ya usafirishaji wa waendesha bodaboda.
- Natoa wito mshirikiane kwa karibu na vyombo vilivyopo kisheria vinavyosimamia sekta yenu.
- Vyombo vilivyopo vinavyosimamia sekta hii vipo kisheria na vinatakiwa kusimamia eneo hili la bodaboda kisheria. Sheria inaagiza na kuelekeza msingi wa kufuatwa.
- Uvaaji wa “Helmet” ni jambo la kisheria na pia ni kwa faida ya mwendeshaaji.

### **Ndugu Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda,**

Ni vema mkafuata taratibu za usajili wa chama cha Bodaboda

- Kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii au Maafisa Ushirika

- Muwe na Katiba ya chama chenu ikiainisha malengo ya kuanzishwa chama chenu, aina ya wanachama, idadi ya wanachama na michango yenu mnataka iweje (kila mwezi au kila mwaka).
- Chama chenu kikishakuwepo kwa mujibu wa sheria, ni rahisi kujiendesha na kutambulika shughuli zake na kupata ushirikiano toka Taasisi mbalimbali zikiwemo taasisi za fedha.
- Suala la mikopo litakuwa nafuu kwenu endapo mtakuwa katika ushirika imara, pia historia yenu itaonekana katika kujiwekea akiba. Kwa sababu akiba hiyo ndiyo itasimama kama dhamana yenu wakati wa kuomba mikopo kwenye Taasisi za fedha.
- Natoa wito kupitia chama chenu muweze kuendeleza pale mlipoishia kwa kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya (CHF). Taarifa nilizonazo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilitoa fedha kuwachangia ili muweze kuingia katika mpango huu, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua jambo ambalo nimeona ni vema niwakumbushe kwani ni la faida kwenu.

Napenda kuhitimisha kwa kuwatekieni kila la kheri kwa shughuli mnazofanya kila mmoja awe balozi wa mwenzake wa kufuata sheria, taratibu na miongozo iliyopo, ipo kwa mujibu wa sheria hivyo kutoifuata ni kukiuka sheria, na yeyote anayekiuka anakuwa amevunja sheria, kuna maelekezo ya namna ya kushughulika na wote wanaovunja sheria.

Mwisho naendelea kuwashukuru watoa mada wote na ninapenda kuwashukuru pia washiriki wa mafunzo haya. Ni matumaini yangu kuwa kutakuwa na tofauti kubwa kwa ninyi mliopata mafunzo na wale ambao

hawajapata mafunzo. Ninyi mliopata mafunzo mtaendesha bodaboda na mtafanya biashara hii ya bodaboda kwa uweledi na nidhamu ya hali ya juu.

Asanteni kwa kunisikiliza.

ZELOTE STEPHEN ZELOTE  
**MKUU WA MKOA**  
**RUKWA**